**Brief No. 6**

# SPECIAL PURPOSE VEHICLE (SPV)

Mradi wa kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji (LIC) ni mradi wa kuendeleza sekta binafsi unaofadhiliwa na Danida. Mradi unashughulikia vikwazo vikuu vinavyokwamisha maendeleo ya biashara na ukuaji wa uchumi katika ngazi ya wilaya kwenye mikoa miwili ya Dodoma na Kigoma nchini Tanzania. LIC imejikita katika mijadala kati ya sekta ya umma na sekta binafsi, miundombinu ya utoaji wa huduma za biashara ikiwa ni pamoja na vituo vya pamoja vya biashara na miundombinu ya pamoja kati ya sekta ya umma na sekta binafsi ili kusaidia maendeleo ya biashara na uwekezaji. Washirika wanaotekeleza mradi wa LIC ni Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Sekretariati za mikoa ya Kigoma na Dodoma, Baraza la Taifa la Biashara (TNBC) Tanzania, Jumuiya ya Tawala za Mitaa Tanzania (ALAT), Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF), Chemba ya Wafanyabiashara, Wenye Viwanda na Kilimo Tanzania (TCCIA).

## Uwekezaji wa miundombinu ya pamoja (PPP) unaosaidia maendeleo ya biashara

LIC imesaidia ukarabati wa maendeleo ya masoko, sehemu za minada, machinjio, masoko ya samaki, miradi ya umwagiliaji, vituo vya mafunzo ya kilimo, usambazaji wa maji na kubuni vituo vya biashara, mpango wa matumizi bora ya ardhi ikiwa ni pamoja na kupata hati miliki na vifaa vya usindikaji mdogo. Uwekezaji huu wote unalenga kushughulikia vikwazo vinavyotambuliwa kupitia mchakato wa majadiliano kati ya sekta ya umma na sekta binafsi kwenye mabaraza ya biashara ya wilaya na mkoa.

## Changamoto za uwekezaji wa pamoja (PPP)

Usimamizi wa zana za umma katika kusaidia maendeleo ya biashara ni kikwazo kikubwa hasa katika ngazi ya serikali za mtaa kutokana na vikwazo mbalimbali; bajeti ya serikali za mtaa ni ndogo sana, watumishi husika kuwa wachache na urasimu wa taratibu za serikali hautoi ushirikiano katika kuleta mabadiliko yanayohitajika kwenye utendaji. Sehemu za kutoa huduma kama masoko na mialo ya samaki ni chanzo cha mapato kwa serikali za mitaa, lakini matengenezo na maboresho katika vyanzo hivi vya mapato hayajapewa kipaumbele stahiki inayopelekea kushuka kwa viwango vya huduma.

Moja ya jibu rasmi kwa changamoto hizi inaweza **kuwa na mfumo wa (SPV)** ambao unajumuisha wajibu wa sekta ya umma katika kutoa huduma na kukusanya mapato huku taratibu na ufanisi wa usimamizi ukifanywa na sekta binafsi.



Picha ya juu ikionyesha Mwalo wa Kibirizi, Kigoma Ujiji



Wafanyabiashara katika mwalo wa Kibirizi, Kigoma Ujiji

## Dhana na utekelezaji wa usimamizi wa chombo cha SPV

Special Purpose Vehicle (SPV) inaweza kutumika kwa ufanisi katika kusimamia miradi ya pamoja (PPP) kama ilivyoonyeshwa katika ukarabati na usimamizi wa soko la samaki la Kibirizi lililoko mkoani Kigoma kwa usaidizi wa LIC. Kampuni binafsi yenye ukomo wa dhamana imeanzishwa ili kusimamia uwekezaji na kukusanya mapato kwa sheria ndogo za serikali za mitaa. Kampuni inachukua majukumu yote yanayohusiana na shughuli za soko na matengenzo na inawajibika kwa bodi ya wakurugenzi ambayo inajumuisha wadau kutoka sekta ya umma na sekta binafsi.

Halmashauri husika inabaki kuwa mmiliki wa kituo cha kutoa huduma na mkataba kati ya kampuni itakayoendesha SPV na serikali inaweka vigezo ambavyo mfumo wa SPV utafuata katika kufanya biashara pamoja. Makubaliano ya jinsi ya kugawanya makusanyo ya mapato pia yanaainishwa kwenye mkataba huo.

Mkurugenzi wa SPV na wasimamizi/wafanyakazi wengine watakaohitajika wanaajiriwa na bodi ya SPV. Menejimenti ya SPV inaajiri wakusanya mapato, walinzi na watumishi wengine watakaohitajika. Uongozi wa SPV unaandaa bajeti ya uwekezaji na uendeshaji ambayo inapitishwa na bodi ya SPV.

Kwa upande wa Kibirizi mkataba unasema kwamba mapato yanayokusanywa yanagawanywa nusu kwa nusu kati ya kampuni inayoendesha SPV na Manispaa ya Kigoma Ujiji (KUMC) baada ya kutoa gharama za uendeshaji kama matengenezo, umeme, maji na ulinzi. Uhalali wa gawio la asilimia 50 kwa kampuni ya SPV ni kwasababu ya uhitaji mkubwa wa ukarabati kama ilivyoelezwa katika mpango kazi uliopitishwa na kwenye bajeti ya SPV. Mgawanyo huu wa mapato unaweza kupitiwa kila mwaka, kwa mashauriano au majadiliano kwasababu SPV sio kampuni ya kutengeneza faida.

Wakusanya mapato wameajiriwa kwa mkataba kwa makubaliano ya kwamba asilimia 20 ya mapato yanayokusanywa yanabaki kwao kama malipo. Wakusanyaji wote wanatumia mashine za kieletroniki za kukusanyia mapato (Point of Sale machines) zinazoangaliwa na uongozi wa SPV na bodi.

Mbali na kuchukua wataalamu kutoka sekta binafsi kuwa wasimamizi, bodi ya SPV inaweza kuleta kundi la wadau mbalimbali ili kuweka wigo mpana na kuhakikisha kuna uwekezaji mkubwa, ufanisi katika ukusanyaji wa mapato huku utoaji huduma ukiimarika. Kwa upande wa machinjio ya ng'ombe, bodi ya SPV mbali na kuleta wawakilishi kutoka serikali za mitaa, inaweza ikaleta wafugaji wa ng'ombe, wafanyabiashara na wawakilishi kutoka kwenye jamii husika kuwa sehemu ya wadau. Mgawanyo wa majukumu katika uwekezaji wa pamoja (PPP) unaongeza uwezekano wa uwekezaji endelevu.

Zaidi ya hayo, kuanzishwa kwa SPV kunaweza kusaidia kampuni hiyo ya SPV kukopesheka na benki ili mradi tu kampuni izingatie makubaliano yaliyopo kwenye mpango wa biashara.



Jengo la ofisi ya kampuni (spv) ndani ya mwalo wa Kibirizi.



Mkusanya kodi katika mwalo wa Kibirizi, Kigoma Ujiji

**Hatua zinazopendekezwa kufuatwa na mradi wa LIC katika utekelezaji wa SPV**

Baada ya ruhusa/idhini kutoka kwenye mradi wa pamoja (PPP) utaratibu ufuatao unaweza kutumiwa na LIC kama kigezo cha kutoa msaada.

1. Makubaliano (MoU) kati ya serikali za mitaa/wanufaika na LIC juu ya nia ya kuanzisha SPV ili kuendesha mradi unaotakiwa kusainiwa.
2. Bodi ya wakurugenzi ya SPV kuchaguliwa/kuteuliwa/kupigiwa kura
3. SPV kusajiliwa, uongozi/menejimenti kuajiriwa na mkataba wa makubaliano ya uendeshaji utengenezwe na uidhinishwe na serikali za mitaa na bodi za wakurugenzi.
4. Menejimenti ya SPV kumaliza mpango wake wa uwekezaji kwa kufuata muongozo wa bodi, kuitwa kwa zabuni, kusainiwa kwa mikataba na kuangalia ujenzi na ukarabati kulingana na ushauri wa kiutalaamu kutoka kwa wafanyakazi wa halmashauri husika
5. Baada ya kuanza kwa shughuli menejimenti ya SPV inaajiri wakusanya mapato na wafanyakazi wasaidizi wanaohitajika
6. Asilimia 20 ya mchango wa serikali za mitaa /wanufaikaji wa mradi iliyoelezwa katika muongozo wa LIC inaweza kutolewa na LIC kama mkopo na kulipwa kwenye mfuko ili kusaidia maendeleo ya kongano/mnyororo wa thamani. Kwa sasa mfumo huu pendekezwa haupo katika mwongozo wa SIFF.

**LIC** imewekeza takriban kiasi cha shilingi za Kitanzania bilioni 5 katika miradi ya pamoja kati ya serikali na sekta binafsi (PPP) kwa mikoa ya Kigoma na Dodoma.

Kwa taarifa zaidi, tafadhali tembelea tovuti ya mradi wa LIC: www.lic.or.tz

**Novemba 2018**